

# Ukweli Kuhusu Chanjo za COVID-19

## Chanjo ni moja wapo ya njia tunayo tumia kupambana na janga la COVID-19



Ili kukomesha janga hili, tunahitaji kutumia njia zote za kuzuia. Chanjo ni moja wapo ya njia bora zaidi ya kulinda afya yako na kuzuia ugonjwa huu. Chanjo hufanya kazi na kinga asili ya mwili wako ili mwili wako uwe tayari kupambana na virusi ikiwa utaambukizwa. Hatua zingine kama kuvaa mask ama barakoa inayofunika pua na mdomo na kukaa angalau futi sita ama mita mbili kutoka kwa watu wengine ambao hauishi nao pia husaidia kuzuia kuenea kwa COVID-19.

Uchunguzi unaonyesha kuwa chanjo hizi ni bora zaidi kwa kuzuia COVID-19. Wataalamu pia wanasema kuwa chanjo hizi za COVID-19 zitasaidia kuzuia kuwa mgonjwa zaidi hata ukiambukizwa. Chanjo hizi haziwezi kukupa ugonjwa wenyewe.



**Chanjo ni salama.** Shirika linalohusika na usalama wa chanjo Marekani limehakikisha kuwa chanjo hizi ni salama iwezekanavyo. Chanjo za COVID-19 zimepitia vipimo vya usalama sawa na chanjo zingine zote.




**Aina tofauti za chanjo za COVID-19 zitapatikana.** Chanjo nyingi zinahitaji kudungwa mara mbili, kila moja kwa wakati tofauti. Chanjo ya kwanza inatayarisha mwili wako. Utapewa chanjo ya pili angalau baada ya wiki tatu ili kuhakikisha una ulinzi kamili. Ikiwa umeambiwa unahitaji chanjo mbili, hakikisha kwamba unapata zote mbili.



Chanjo zinaweza kusababisha athari kwa watu wengine, kama misuli kuuma, uchovu, au homa kali. Athari hizi zinamaanisha chanjo inafanya kazi kusaidia kufundisha mwili wako jinsi ya kupambana na COVID-19. Kwa watu wengi, athari hizi hazitadumu zaidi ya siku moja au mbili. Kuwa na aina hizi za athari hazimaanishi kuwa una COVID-19. Ikiwa una maswali juu ya afya yako baada ya chanjo, piga simu kwa daktari wako au kliniki. Kama ilivyo na dawa yoyote, unaweza kupata athari mbaya kama vile kutoweza kupumua, lakini hii si kawaida. Ikiwa itafanyika, piga simu 911 au nenda kwenye hospitali.



**Unapopata chanjo, hakikisha kuwa wewe na yule anayekuhudumia mumevaa mask ama barakoa.**



**Hata baada ya kupata chanjo yako, endelea kuvaa mask ama barakoa, kunawa mikono mara nyingi, na kukaa angalau futi sita mbali kutoka kwa watu wengine ambao hauishi nao.**

Hivi sasa, haijulikani chanjo hizi zitakulinda kwa muda gani, kwa hivyo ni vizuri kuendelea kufuata maagizo kutoka kwa CDC na idara ya afya. **Sio kila mtu atapata chanjo kwa wakati moja, kwa hivyo bado ni muhimu kujilinda kutokana na wengine.**<sup>1</sup>

<sup>1</sup> This information sheet, dated 1/23/2021, is a redraft and retranslation of a document dated 1/13/21 and originally prepared by The National Resource Center for Refugees, Immigrants, and Migrants (NRC-RIM). This retranslation was completed by Dillon Mahoney, Renice Obure, Mathews Wakhungu, and Eugenie Umurutasate of the University of South Florida. For information, contact dmahoney1@usf.edu.